**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 02 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**

156. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuimarisha Jiji la Zanzibar kupitia miundombinu imara. Pamoja na juhudi hizo nzuri bado yapo baadhi ya maeneo ya ndani ya mitaa yetu

yanakabiliwa na kiza wakati wa usiku na kupelekea wahalifu kutumia mwanya huo kufanya vitendo viovu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka nguzo za taa ndani ya mitaa yetu ili kuimarisha usalama na kudhibiti vitendo vya uhalifu hasa nyakati za usiku.

(b) Je, Kuna uwezekano wowote kupitia bajeti ya mwaka huu (2021/22) Serikali ikaweka taa hizo kwa kuanzia na mitaa ya Jimbo la Kikwajuni.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

14. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Visiwa vya Unguja na Pemba vinatembelewa na wageni wengi kutoka maeneo mbali mbali duniani. Kwa kuwa usafi ni muhimu kwa binadamu wote ikiwa ni pamoja na wageni wanaofika Zanzibar. Na kwa kuwa miongoni mwa maeneo yanayohitaji usafi ni vyoo. Na kwa kuwa katika miji midogo ya Pemba hakuna vyoo vya Manispaa wala watu binafsi vya kulipia, jambo linalopelekea wageni kujisaidia katika maeneo hatarishi.

Je, ni lini Serikali itaamua kujenga vyoo vya kulipia katika maeneo ya miji ya Pemba ili wageni wapate stara wanapotembelea katika miji yetu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

209. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika kuendeleza shughuli mbali mbali zinazofanywa na Wizara yako, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inasaidia sana kuratibu na kutoa matokeo mazuri ya utendaji wa Wizara.

(a) Je, tafiti ngapi zinazohusiana na ajira kwa vijana zimefanywa na wizara yako.

(b) Je, tafiti hizo zimetoa matokeo gani.

(c) Je, Serikali imechukuwa juhudi gani kutokana na matokeo ya tafiti hizo ili vijana wajuwe jitihada ya Serikali yao.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

178. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika msimu uliopita wa uchumaji wa karafuu, kuna baadhi ya wananchi walioanguka mikarafuu na mpaka sasa hivi hawajalipwa fidia zao.

(a) Je, Wizara inalifahamu suala hili.

(b) Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

140. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika Hospitali ya Rufaa Mkoani kuna vifaa vya uchunguzi wa vinyama (Tissue) ambavyo vina umuhimu mkubwa katika kufanikisha utendaji wa kazi za kila siku hospitalini ambapo kwa sasa hakuna mtaalamu wa kuweza kuvifanyia kazi.

Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalamu wa vifaa hivyo (Hystopathology) ambaye uwepo wake utarahisisha shughuli za matibabu hospitalini hapo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

162. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kufahamu kuwa kiwanja cha ndege cha Pemba ni moja ya viwanja muhimu sana katika kuimarisha maendeleo ya Zanzibar. Serikali imepanga kuendeleza mchakato wa ujenzi wake ili kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana, kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025.

(a) Je, Serikali imepanga kuajiri vijana wangapi hadi

kukamilika ujenzi huo.

(b) Je, katika ajira hizo ni ajira ngapi za kudumu na ajira ngapi zinatarajiwa kuwa za mikataba.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

198. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wa Jimbo la Nungwi ni wakulima wakubwa wa mazao ya muhogo na viazi vikuu lakini wanahitaji kutiwa motisha na Serikali yao.

Je, ni lini utakuja kuwatembelea na kuangalia maendeleo yao pamoja na kuwasikiliza changamoto zao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

91. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Haki ya kupata fedha za likizo ni ya kila mfanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na walimu. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko ya walimu hao kutolipwa fedha za likizo zao.

Je, kwa nini walimu hawapati fedha zao za likizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

195. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Miongoni mwa changamoto inazozikabili Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) ni pamoja na kuwepo kwa ongezeko la madeni kwa taasisi za Serikali, hali inayolipelekea Shirika kupunguza mapato yake.

(a) Je, kuna kikwazo gani kwa taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni yao licha ya taasisi hizo kupitishiwa bajeti zao kila mwaka.

(b) Je, Serikali italisaidia vipi Shirika ili madeni wanayodai kwa taasisi mbali mbali za Serikali yaweze kulipwa.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2021/2022.

| | |
|---|---|
| **Zanzibar,** | **(Raya Issa Msellem)** |
| **02 Juni, 2021.** | **KATIBU WA BARAZA** |